

| | |
|---|-------------------|
| Mielekeo ya Kifikra katika Hadithi Fupi Kwa Mwandishi wa Tanzania Mwinda Mbatiah | العنوان: |
| مجلة كلية اللغات والترجمة | المصدر: |
| جامعة الازهر - كلية اللغات والترجمة | الناشر: |
| Abdul-Maqsuud, Khalid Bakriy | المؤلف الرئيسي: |
| ع8 | المجلد/العدد: |
| نعم | محكمة: |
| 2015 | التاريخ الميلادي: |
| يناير | الشهر: |
| 122 - 150 | الصفحات: |
| 752884 | رقم MD: |
| بحوث ومقالات | نوع المحتوى: |
| Unknown | اللغة: |
| AraBase | قواعد المعلومات: |
| النقد الأدبي، القصص القصيرة العربية | مواضيع: |
| http://search.mandumah.com/Record/752884 | رابط: |

Mielekeo ya Kifikra katika Hadithi Fupi

Kwa

Mwandishi wa Tanzania Mwindi Mbatiah

Utafiti Umeandaliwa na

Dkt Khalid Bakriy Abdul-Maqsud

Profesa Msaidizi wa Fasihi ya Kiswahili

Kitengo cha Lugha za Kiafrika

Kiswahili

Utangulizi:

Hadithi Fupi inazingatiwa ni miongoni mwa elementi muhimu katika Fasihi ya Kiswahili kwa ujumla, na katika Nathari kwa sifa maalumu. Na waandishi wa Hadithi Fupi wamefanya juhudi kubwa ya kuandaa na kuweka misingi ambayo inapangilia Sanaa hii ya Fasihi ambayo inaambatana na hali ya mazingira ya kisasa na maendeleo yake yanayofuatana na ambayo yanahitajia kufupishwa na kukatisha. Na atakaetazama kitabu cha "Misingi ya Hadithi Fupi" ⁽¹⁾ atakuta kuwa kimejaribu kuweka historia ya sanaa hii ya nathari na kuweka misingi yake. Na kimetumia mifano ya waandishi wakubwa wa Kiswahili ambao wametoa mchango wao kupitia Hadithi zao wakionesha mitazamo yao kwa jamii na matatizo yake.

Na Msekele hakuwa peke yake ambae amekuwa na shime ya Hadithi Fupi, kuna waandishi wengi na wahakiki walikuwa na shime katika vitabu vyao na tafiti zao ambazo ziliandika nathari ya Kiswahili uliodhihirika kutoka katika vitabu ambavyo Hadithi Fupi ilijipatia nafasi ya kutosha ndani yake⁽²⁾, kama ambavyo baadhi ya Wahakiki wa Sanaa hii pia walikuwa na shime pia kupitia baadhi ya kamusi zao ambazo ziliandika namna ya kuweka mweleweko maalumu wa Sanaa hii na kupangilia Misingi yake. ⁽³⁾

Na kwa wakati huo huo, baadhi ya vitabu ambavyo vinabeba ndani yake Hadithi fupi, vya waandishi mbali mbali, vilianza kujitokeza katika medani ya Fasihi. Na miongoni mwa vilivyo safu ya mbele ni vile vitabu vya Fasihi kama vile Mwendawazimu na Hadithi Nyingine, na kilichapishwa na Kampuni ya Jomo Kenyata Foundation, mwaka wa 2000, na Mbatiahh ndiye aliyehusika na

usimamizi wa kukitoa kitabu hichi cha Fasihi ambacho kilikuwa na Hadithi Fupi Kumi za mkusanyiko wa Vitabu vya Nathari ya Kiswahili.

Na mwaka wa 2007, kikatolewa kitabu cha "Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine", chenye mkusanyiko uliochaguliwa vyema kutoka katika vitabu vya Hadithi Fupiza Kiswahili, na kilikuwa na Hadithi Kumi na Mbili na kilisimamiwa na Focus Publisher, L.T.D, huko Nairobi na Mbatiah pia akasimamia Uchapishwaji wa Kitabu hiki.

Na katika kipindi hicho hicho kampuni ya East African Educational Publishers L.T.D, huko Nairobi ikatoa Diwani ya "Alidhani Kapata" na ikawa na Hadithi Fupikumi na nne, ambapo aliesimamia utolewaje wake alikuwa: P.L. Iribemwangi, na Mbatiah alichangia katika Diwani tatu kwa Hadithi Fupisita na zilikuwa kama ifuatavyo:

1- Mwendawazimu na Hadithi Nyingine alichangia kwa Hadithi Fupitatu:

- A. Arusi
- B. Kiumbe Huchukuliki
- C. Uperesheni Kipindupindu

2- Katika Diwani ya Kurudi Nyumbani, Mbatiah alichangia kwa Hadithi Fupi mbili tu:

- A. Ngozi ya Mtu Mweupe.

B. Kurudi Nyumbani

3- Na katika Diwani ya Alidhani Kapata, alichangia kwa Hadithi Fupimoja iitwayo Sami.

Ni jambo zuri iwapo tutataja kwamba Mbatiah ndiye mwandishi pekee wa katika Vitabu hivi vitatu vya Diwani ambaye aliandika Hadithi Fupi sita, na hii ni idadi ambayo hakuna mtu yeyote mwingine aliyeweza kuifikia miongoni mwa waandishi wa wengine wa Diwani Hizi tatu, na katika jambo hili kuna ishara ya shime yake katika Sanaa hii na utashi wake katika kutoa mchango wa maendeleo na kustawi kwake.

Mbatiah katika Hadithi hizi Fupi, ameandika kuhusu mambo ambayo aliyaona kuwa yanafaa kutafutiwa ufumbuzi wake kwa njia ya Fasihi. Na sisi kwa mchango wetu, tutajaribu katika utafiti huu, kuangazia juu ya mielekeo ya kifikra ambayo ilijitokeza kupitia utatuzi wake wa masuala hata ambayo mielekeo hiyo ilijihusisha nayo, na kujaribu kuchambua kwa uchambuzi wa kifasihi unaotumia juu ya namna mwandishi alivyoyashughulikia masuala haya muhimu ambayo yanayagusa maisha ya watu, kuanzia majukumu yake kama mwandishi na mwanafasihi anaehusisha na masuala ambayo yanatokea katika jamii ambayo anaishi ndani yake, na anachanganyika nayo pamoja na masuala yake. Na miongoni mwa mielekeo iliyo mbele na ambayo ilijitokeza katika Hadithi hizi ni kama ifuatavyo:

Familia ya Mbatiah.

Familia ina nafasi kubwa katika Hadithi Fupiza Mbatiah, kwa hivyo ameelezea hali ya Familia na matatizo yake kwa kuamini uwepo

wa mchango muhimu na nyeti ambao utapelekea kumea kwa kila mtu katika jamii, na akaonesha mazuri ya Mfahamiano na Uelewano kati ya wanajamii na mabaya Chuki na Magomvi. Na Hadithi yake ya "Arusi" ilikuwa ni moja kati ya Hadithi zilizoandika ndani yake kuhusu sura ya Familia kupitia mazungumzo yaliyofanyika kati ya Baba na Mwanae wa kiume ambae alimuomba mzazi wake ampe nasaha kuhusu kutaka kumuoa msichana mmoja, na baba yake akamnasihwa kwa jinsi alivyoona kuwa ni kwa masilahi yake na masilahi ya familia kwa ujumla. Isipokuwa Mtunzi hapa, ameunda sura ya Baba kama mlezi wa Familia ambae ametoa nasaha hiyo kwa mwanane kwa sura ya ukali ambapo mtoto hakutosheka nayo au hata kuipokea na kuikubali nasaha hiyo na pamoja na kuwa baba ni mtu mwenye uzoefu na majaribio, isipokuwa hakufanikiwa kumjua mwanae na kumkinaisha kutokana na ombi lake la kutaka kumuoa msichana wa sehemu ya jamii inaloamini uchawi na ulozi. Msichana ambaye hakuna kijana yeyote aliyewahi kuthubutu kujaribu kutaka kufunga nae ndoa isipokuwa alipatwa na madhara makubwa mno, na akamalizia nasaha yake kwa onyo kali kama ifuatavyo:

"Ukiyapuuza hayo niliyokwambia, sitakuwa na jengine la kufanya ila kujisema tu kwa anayepuuza ushauri wa wazee baraka zao humpuuza".⁽⁴⁾

Onyo la Baba kwa mwanae halikuwa mwisho wa mazungumzo, Mtunzi alijenga sura ya jibu kali kwa mtoto kutokana na kitisho hichi alichokitoa Baba, na akasema: "Ulimwengu umebadilika na umeangazwa kwa nuru ya elimu ... Uchawi una thamani gani katika Dunia ya leo kama ilivyo?"⁽⁵⁾

Jibu hili halikumpendeza Baba ambaye hakuweza kuvumilia mjadala, na jibu lake likawa linawakilisha kilele cha ugomvi wa kifikra kati ya vizazi viwili;

Kwanza: ugomvi huu unawakilishwa na Baba anaeamini mila na desturi zilizorithiwa na kuzijali:

Pili: unawakilishwa na mtoto ambae haamini hivyo na wala hajali isipokuwa elimu ya kisasa ambayo ni lazima iongoze jamii na kutawala mawazo ya watu. Na jibu la Baba kwa mwanae na jibu la mtoto kwa baba yake yalikuwa kama ifuatavyo:

Baba akasema kwa hasira: "Ukimwoa wewe si mwanangu tena, mzee alifoka, ukinikataza kumwoa, basi wewe si babangu tena, Miriti alitamka kwa hamaki" ⁽⁶⁾.

Hii Sura ya ukali wa mazungumzo kati ya Baba na Mwanae. Mtoto hakuelewa nasaha ya Baba yake aliyepatwa na hofu juu ya mwanae, na Baba ambaye hakuweza kuvumilia mazungumza na mwanae pamoja na hoja na dalili zake alizozitoa ambazo zililenga kuutetea muono wake, na huu ulikuwa mwisho mbaya kwa mtoto ambae alifariki dunia kwa ajali iliyotokea siku ya harusi yake alipomuoa yule msichana ampendae ambae alikataliwa na Baba yake. Na hii ni kama ishara ya mwandishi ya kuuona umuhimu wa kuelewana na kufikia makubaliano ya pamoja kati ya pande mbili za familia; Baba na Mwanae, ili mwisho wa tofauti hizi usiwe wa kusikitisha kama ilivyotokea mwisho wa Hadithi hii.

Na katika Hadithi ya pili; "Kiumbe Hauchukuliki" mwandishi ameandika kuhusu sura ya Familia yenye Mume ambaye ni Kibunga,

na Mke ambaye ni Muthoni, aliyekuwa mwimbaji katika moja ya vilabu –na Kibunga akataka kumuoa na wakakubaliana kujenga familia mpya yenye msingi wa kuheshimiana na matumaini kwa maisha bora ya siku za usoni, na akajaribu kumlea mtoto wa Muthoni ambaye Kibunga alimkubali na kumzingatia kama mwanae wa kufikia– na mwandishi hapa, amejenga sura ya athari za ujenzi wa familia zilizojitokeza katika maisha ya; ambapo aliendesha maisha yake ya kawaida kama mke na mama, anabeba majukumu yake.

Mwandishi huyu amejenga sura ya mwanamke huyu na jinsi watu wanavyomtazama kama mwanamke afanyae kazi katika jumba la starehe kwa namna mwandishi alivyoelezea hisia za mwanamke huyu baada ya hali yake kubadilika, kama ifuatavyo: "Alijiona kuwa ni mtu aliyepewa heshima na watu kila alipopita na kusalimiwa akiitwa Bi Kibunga moyo wake ulijawa na furaha." ⁽⁷⁾

Hii ndio hali yake baada ya kuishi maisha mapya kama nguzo kuu miongoni mwa nguzo za familia, familia hii ambayo, mwandishi ameashiria umuhimu wake katika kuujenga Utu wake, na athari zake katika maisha ya Binadamu na mustakbali wake. Na hii ni pale alipoashiria jaribio la wanakijiji kutaka kuijua sili ya anakotokea yeye, familia yake na watoto wao. ⁽⁸⁾

Sura hii ya familia iliyochorwa na jinsi gani familia hiyo ilichangia kuubadilisha Utu wa Muthoni na kuwa mtu anaeshimika na watu wote wanamjali. Mwandishi aliikamilisha sura hii ya Muthoni pale alipoiunda baada ya kupita kipindi kirefu cha maisha ya ndoa ya familia hii, Muthoni akaanza kupuuzia kazi zake za kifamilia na akaanza kuhisi uwepo wa utashi wa kurejea tena katika maisha yake ya anasa na mchezo baada ya yote haya, na upuuzi huu akamrithisha na mmwanae (Ben), na mwisho wake ukawa ni kifo kilichotokea katika moja ya nyumba za akina mama, na hili ni jaribio la mwandishi kutaka kudhihirisha nafasi ya sababu za Urithi wa kimaumbile na

athari zake katika Utu wa mtu, na baada ya kufariki kwa Mwane wa kiume, mama nae akaiaga dunia mikononi mwa Mwanamke aliyesababisha kifo cha mwanae.

Hivi ndivyo ulivyokuwa mwisho wa mhusika huyu ambaye mwandishi aliweka wazi tangu mwanzo kuwa hakuwa sawasawa, na wala hakuoneaka kwa jinsi alivyo kwamba alikuwa na familia yenye nguvu na iliyokamatana vizuri, inamuhisisha majukumu yake nyumbani kwake na kwa watoto wake, na kwa hivyo huu ulikuwa ndio mwisho wa huzuni wake yeye na wa mwanae baada ya kushindwa kuendana na maisha yake katika familia mpya.

Na Hadithi ya "Ngozi ya Mtu Mweupe", imeundwa sura ya familia inayofanana kwa upande wa idadi, na ni familia yenye Baba, Mama na Mtoto wa kiume, isipokuwa imetofautiana na familia zote ziliyotangulia kwa kuwa yenyewe si ya Kikenya bali ni ya Kiingereza iliyohamia kimaisha nchini Kenya, na kupitia familia hii, mwandishi amezungumzia suala nyeti ambalo ni jinsi mwingereza aionavyo Kenya na Wakenya, na kuwazingatia kuwa Kenya itaendelea kuwa ni nchi ya Mtu mweupe, kwamba wakenya hawako katika kiwango kile kile cha Ubinadamu wa mwingereza, kutokana na mwandishi kuifuatilia sura ya mlezi wa familia Robert Stonheart na Mama Best Ston Hert, na akiwa ni Alla. Na hii ni familia isiyo tulivu kwa sababu ya baba asiyeyajali majukumu yake na wala haheshimu haki za familia. Mwandishi ameijenga sura ya Mlezi huyu wa familia kuwa anamuua mke wake kutokana na mabishano yaliyosababishwa na hasara alizozipata katika biashara yake na akadhani kuwa mke wake ndiye sababu ya yote hayo ⁽⁹⁾, na kwa hivyo, familia ikamkosa mmoja wa nguzo zake muhimu, na ikawa haina familia hiyo isipokuwa baba mwenye mawazo ya kibaguzi, na mtoto anaeona kuwa jambo hili ni kwenda kinyume na akili, mantiki na pia uhalisia.

Baba yule ambaye alijenga sura ya hali isiyomuheshimu mwanamke moja kwa moja kuwa mwanamke ni kiumbe Shetani. ⁽¹⁰⁾ na huyu ndiye yule Baba ambaye alijaribu kuuhamishia mgogoro wake wa kifikra kwa mwanae, isipokuwa mwanae huyo akiwa katika hali ya tulivu na kwa kutumia akili, alimjibu baba yake kwa

kumwambia: "Nilimwonesha kuwa mimi sasa nilikuwa mtu mzima, huru".⁽¹¹⁾

Haukuzuka mgogoro kati ya baba na mwanae, lakini mwandishi ameashiria kuwa fikra za baba zilpitwa na wakati, na kwamba watoto wana haki yao ya wao kuwa na mtazamo wao na kujiamulia maisha yao ya siku za usoni.

Mwandishi baada ya hapo, akahamia katika kuzungumzia hadithi mpya inayotofautiana na ile ilichotangulia. Katika hadithi ya "Kurejea Nyumbani", mwandishi aliunda sura ya familia yenye baba, mama, mtoto wakike na mtoto wa kiume, isipokuwa uzingatiaji zaidi ulikuwa katika uhusiano unaowafungamanisha baba na mwanae wa kiume, na mwandishi akazungumzia namna ya kuimarisha thamani ya familia kati ya wanandugu ndani ya nyumba moja vyovyote hali itakavyokuwa, na hili ni kama alivyolijenga mwandishi katika maelezo yafuatayo:

"Jambo moja ambalo wazazi wangu walihakikisha kwa limezama katika akili za watoto wao wawili ni kuwa nyumbani kwetu ni Meru,"⁽¹²⁾

Baba amezingatia kuwa nyumba iliyopo ni ya familia katika mji wa Meru, nayo ni nyumba kubwa ya familia ambayo inawakusanya wanandugu wote, hata kama baadhi yao watatawanyika hapo baadae katika maisha ya kikazi, mwisho wa yote, nyumba hii ndio kitovu cha familia.

Mfungamano huu wa kifamilia ulijitokeza pale mama alipoumwa na kulazwa hospitalini, mwandishi alijenga sura ya familia hii na anasema: "Mimi na kambi na babangu tulikuwa tunakwenda kumuona kila siku".⁽¹³⁾

Sura ambayo ina uelewano na upendo kati ya wanandugu wa familia iliyo sawa katika hali ya mmoja wao kuugua na hasa hasa mama. Mwandishi akaendelea baada ya hapo akielezea hisia mtoto wa kiume kwa mama yake huyu pale alipoambiwa yeye pamoja na baba yako kuwa hali ya mama yake ya kiafya inazorota, akasema akielezea

hisia zake kwamba: "Mama amekufa, maneno hayo yalipita akilini mwangu kama mwale wa radi".⁽¹⁴⁾

Hivi ndivyo mwandishi alivyoielezea hali ya yule mtoto wa kiume pale mtoto huyo alipojua hali ya mama yake kiafya. Na mwandishi pia hakuacha kuielezea hali ya kijana huyo alipokuwa akiielezea hali ya mama yake kwa kauli yake "masikini mama yangu, masikini mama yangu mpendwa"⁽¹⁵⁾

Na haikuwa hii ni hali ya mtoto huyo wa kiume peke yake, bali pia mwandishi alileta sura ya baba kwa maneno ya mwanae akisema: "Uso wa babangu ulichukua sura ya mzee wa miaka sitini, nilimhurumia ulimwengu wangu mwenyewe umeporomoka".⁽¹⁶⁾

Hisia hizi za huyu mtoto hazikuwa isipokuwa yeye alihisi kuipoteza moja kati ya nguzo nyeti za familia, naye ni mama mzazi ambaye yeye na mume wake walikuwa wakiwakilisha akili zilizokomaa kwa mtoto huyo na wenye ari ya maisha yake ya baaadae, akasema mwandishi huyu alkiielezea hali hiyo ya baba: "Sisi kama wazazi wako, tuna majibu ya kufanya uamuzi katika hali kama hii".⁽¹⁷⁾

Hii ni sura ya familia ya kawaida ambayo wanandugu hushirikiana katika kupitisha maamuzi magumu ya mwelekeo wa wote. Ni ukamilishanaji ambao ameuonesha mwandishi kati ya baba na mwanae, na nafasi ya mama katika kumsaidia mwanae akubali nasaha ambayo hapaswi isipokuwa kuwa na uhakika wa maisha ya baadae ya mwanae akisema: "Na sisi wazazi wako tutakupua baraka zetu".⁽¹⁸⁾

Na hivi ndivyo ushirikiano kamili kati ya mchango wa mama na wa baba katika familia ulivyokuwa, na ambao ulimwezesha mama baadae kuweza kumwelekeza mwanae kwa maelekezo mazuri kwa ajili ya maisha yake ya baadae.

Baada ya hapo, mwandishi akahamia katika kuzungumzia hadithi fupi nyingine mpya "Sami", ambapo alizungumzia ndani yake familia ya baba, mama na mtoto wa kiume. Na mtutu huyu wa kiume

ni muathirika wa ukimwi. Na mwandishi akazungumzia machungu na mateso ya baba na mama walio mafakiri, katika kumtibu mtoto wao huyu mwenye ukimwi, na mwandishi akaelezea hisia za baba na mama kwa mtoto wao huyu. Akaunda sura ya baba mwanzoni, akiwa hana la kufanya kwa ufukara wake alionao, lakini pamoja na hayo, hachoki wala hafanyi uzembe wa kusaka njia ya kumtibu mwanae hata kama tiba hiyo itakuwa juu ya uwezo wake, na akataja hali ya baba aliyepatwa na huzuni kutokana na uzembe anaokutana nao mwanae katika hospitali ya serikali, ingawa baba ni fukara, lakini alijaribu kumtafuta daktari, kama asemavyo: "Alimtafutia daktari ambaye alikuwa na kliniki ya binafsi mjuni".⁽¹⁹⁾

Maelezo yaliyotangulia yamezionesha hisia za Baba, mlezi wa familia kwa mwanae mgonjwa katika tiba kumtibu, na mwandishi hakupitwa katika kuelezea hali ya mama na hisia zake nyingi kwa mwanae, na kwa hivyo, baba akasukubmwa na mama ili aende kukopa fedha ili anunue dawa ambayo itamtibu mwanae huku akitoa sababu za kufanya hivyo kwamba wao ingawa ni mafukara isipokuwa wako tayari kulipa deni lao pale hali itakapokuwa nzuri.⁽²⁰⁾ Na daktari wa mtoto wao alipong'ang'ania kwamba mtoto lazima akiri mbele ya halaiki kuwa ana ugonjwa wa Ukimwi na ashiriki kwa juhudi zake binafsi katika kupambana na usambazaji wake, na akalizingati hili kuwa ni sharti la mtu kutibiwa bure, mama alikataa kata kata na akasema: Haiwezekani ... tumeaibika vya kutosha",⁽²¹⁾

Familia hii inachelea juu ya mtoto wake kutokana na fedheha iwapo ugonjwa wake ungetangazwa hadharani, mwandishi amejenga, huku inahisi furaha iwapo kitu chochote kitapatikana na kusaidia matibabu ya mtoto huyu, kwani pale alipokuja mmoja kati ya marafiki wa mtoto huyo huku akiwa na fedha zitakazosaidia katika matibabu, mwandishi akajenga sura ya furaha ya familia hii kwa kusema: "Wazazi wake walifurahi na kusikia hivyo".⁽²²⁾

Hii ni sura ya familia inayomuogopea mtoto wake na ambayo inafanya kila kinachowezekana ili atibiwe. Na mwandishi akamfanya mtoto huyu ambae amelelewa na wazazi wake wawili, kuwa ni mtu msamehevu, ana maadili mema na heshima kwa wingi. Na baba alihisi

jukumu lake kwa yale yaliyompata mwanae, na mwandishi akajenga picha ya mtoto akikanusha jambo hilo na kuelezea yaliyotokea kuwa huwenda yakawa yamesababishwa na bahati mbaya tu, ili baba asijihisi jukumu lolote kwa yaliyotokea.

Mbatiah na Elimu.

Mbatiah alikuwa na ari ya kujali elimu na akaiashiria mara kwa mara katika Hadithi zake fupi, na jambo hili ni kwa kuwa elimu ni miongoni mwa maudhui zenye kuathiri maisha ya baadae ya mama yeyote yule. Na ingawa mwandishi alilizungumzia jambo hili, haikuwa katika Hadithi maalumu kwa ukamilifu, kwa hivyo zikuta zikirejea rejea ndani ya Hadithi za na kuthibitisha utashi wa kutaka kuonesha umuhimu wa suala hili na athari zake za moja kwa moja juu ya uma hivi sasa na siku za usoni.

Katika Hadithi ya Arusi ⁽²³⁾ mhusika mkuu alikuwa akifanya kazi katika Nyanja za elimu, na hii ni katika njia alizozitumia mwandishi kuashiria umuhimu wa kazi hii.

Lakini baada ya hayo, katika suala lifuatalo, mtazamo wa Mbatiah ulipanuka zaidi, nayo ni Hadithi ya "Kiumbe Hachukuliki", kwani mhusika mkuu pia alikuwa akifanya kazi katika uwanja wa elimu, ndani ya moja ya shule, na mwandishi akaleta mwono wake kwa kazi hii ya ualimu katika sekta hii nyeti kupitia anavyomwelezea Kibunga ambae ingawa anafanya kazi ya ualimu, alikuwa na kazi nyingine zinazomwingizia pato zuri au pamoja na hayo, yeye ana msimamo katika kazi yake kwa mujibu wa maelezo ya mwandishi:

"Bado aliyeng'ang'ania kazi duni ya ualimu? Katika nchi ambao fedha zilipendwa nakutukuzwa zaidi ya chochote kingine, katika nchi ambapo walimu walifanya kazi ngumu na hulipwa malipo duni katika nchi ambao kazi za ualimu ulihusishwa na umaskini". ⁽²⁴⁾

Ukosoaji huu unaelekezwa kwa nguvu dhidi ya nchi isiyojali na kuthamini elimu na wafanya kazi wake, kwa kiwango –kama alivyosema mwandishi– kwamba umasikia umekuwa ukimwandama yeyote anaefanya kazi katika Nyanja hii muhimu ya elimu. Hii sekta

ambayo mmoja wa wafanyakazi ndani yake alikuwa ni mtu muhimu, na akaelezea mwandishi namna anavyojigamba kwa kazi yake na kwa wafanyakazi wengine ndani ya sekta hii, na jinsi mtazamo wake alivyokuwa akijiona na pia watu walivyokuwa wakimuona. Mwandishi alikuwa akibainisha kwamba nchi peke yake haiwezi kuifanya kazi hii nyeti, na akaelezea hayo katika mazungumzo ya kati ya Kibunga na mke wake Muthoni, ambaye alimtaka akeshe katika moja ya majumba ya anasa, na jibu lake likawa kama ifuatavyo:

"Je, hujui kwamba mimi ni mwalimu? Hujui kwamba sisi ni watu wanaoheshimiwa katika jamii?"⁽²⁵⁾

Na huu ndio mtazamo wa mwalimu jinsi ajionavyo, na ni mtazamo wa jamii jinsi imuonavyo na pia kwa sehemu ya jamii anayoiwakilisha. Nao ni mtazamo unaopingana na ule wan chi katika sekta hii muhimu.

Na mwandishi akaendeleza ari yake katika maudhui hii kwenye Hadithi ya "Ngozi ya Mtu Mweupe". Katika Hadithi hii, mwandishi ameonesha ari kwa kuiashiria elimu kwa ujumla lakini pia akatenga sehemu ndogo si mbaya, akizungumzia elimu kwa wasichana, kwa kumzungumzia mhusika Saida ambae alizungumzia hatua za elimu yake, wakati akijibu swali katika mazungumzo, akasema: "Alihudhuria shule moja ya wasichana huko Nairobi, shule hiyo iliwachukua watu wa rangi zote. Alinieleza kuwa kwa wakati huu yenye ndiye aliyekuwa mwafrika wa pekee hapo shuleni, kulikuwa na wahindi waarabu na wazungu wenge, nilishangazwa na hali hiyo, hasa wachache wa waafrika shuleni mwao. Nilitaka kujua maoni yake kuhusu jambo hilo, jibu lake lilikuwa kwamba wasichana waki afrika waliohudhuria shule walikuwa wachache sana. Sio hapo shuleni kwao tu, bali kote chini waafrika wengi walishilikia mila zao zilizoelekea kusema kwamba haikuwa na maana kamwelimisha msichana."⁽²⁶⁾

Ishara iliyopo hapa ni nchi kutowawezesha watoto wake waingie shule na hasa wasichana miongoni mwa watoto hao, na kwamba kila fursa ya elimu iliyo ni kwa wageni tu na si kwa wenyewe wananchi wa asili. Hata kama mwandishi ameibebesha nchi

jukumu, lakini yeye mwenyewe kwa wakati huo huo amewabebesha watu wengine pia jukumu la hali hii; kwani wao bado wanaendelea kuwa na misimamo yao kuendelea mila na desturi za kale ambazo zinaona kuwa hakuna faida yeyote itokanayo na kuwasomesha wasichana. Na hili ni jambo ambalo alijaribu kulikanusha kupitia mhusika Saida ambae alikuwa kutokana na elimu yake, mfano mzuri wa kuigwa.

Ikiwa mwandishi amezungumzia katika sehemu iliyotangulia, elimu kwa wasichana, na akatenga kiasi cha sehemu ambayo si mbaya kwa hili, na hasa katika vipindi vya kabla ya chuo kikuu, yeye katika Hadithi ya "Kurudi Nyumbani", ameuashiria umuhimu wa elimu ya chuo kikuu na mateso ya Gatobu ambaye alipata shida sana mpaka akafanikiwa kwa msaada wa wazazi wake, kuvuka kipindi hichi na kujiunga na taasisi ya Usalama ili afanye kazi kama askari ndani ya taasisi hiyo, baada ya kushindwa kujiunga na Kitivo cha Sheria. ⁽²⁷⁾

Na katika suala la mwisho "Sami", mwandishi amezilungumzia suala la elimu kwa upande mwingine, amezingatia zaidi maswala ya utoro na sababu zake, kupitia mhusika Sami ambae aliielezea hali yake ya kielimu kwa kusema: "Kabla ya kuacha shule, aliyependa sana masomo, lakini kwa bahati mbaya babake alishindwa kulipa karo ikabidi aachie masoma darasa la saba alisikitika sana." ⁽²⁸⁾

Na akaweka wazi sababu kuu za Sami kutokuwa na uwezo wa kukamilisha masomo yake, nazo ni za kiuchumi, zinazotuama kushindwa kwa baba yake kumlipia ada ya shule inayotakiwa ili akamilishe masomo yake. Ingawa mwandishi amemtumia mhusika huyu mwanzoni kwa ajili ya kuashiria athari za hali za uchumi juu ya hali za elimu, mwandishi aliashiria baada ya hayo kwamba si suala linalomuhusu Sami tu bali linawasumbua watu wengi, na akaonesha matokeo yake ambayo ni matatizo ya kijamii yaliyo ya hatari, akasema: "Watoto wengi walipoacha shule waliingia katika shughuli za uhalifu, walianza kuvuta bangi, miraa na kushirikiana na wahalifu waliokomaa." ⁽²⁹⁾

Ashirio lililotangulia linabainisha kuwa matatizo mengi ya kijamii yanasababishwa na moja kati ya sababu za utoro na kutokuwa na uwezo wa wazazi kuwalipia watoto wao ada za shule katika shule hizi. Na huenda katika jambo hili kuna ashirio la umuhimu wa kutafuta utatuzi wa tatizo hili linalowasumbua wengi katika jamii na wanajamii kwa sababu ya kuenea kwake haraka na kutopatiwa utatuzi wake.

Ufisadi:

Miongoni mwa masuala aliyoyashughulikia Mbatiah katika Hadithi fupi, ni Hadithi ya ufisadi, na hiyo, ameitengea Hadithi kamili maudhui hii muhimu ambayo waandishi wa Hadithi Fupikwa Kiswahili, wamekuwa na ari nayo na kuzingatia zaidi ari yao hiyo juu ya ufisadi ambao unafanywa na wanasiasa nchini. Isipokuwa Mbatiah alizingatia zaidi kwa ari yake, juu ya sekta nyingine ambayo ni ufisadi wa wafanyakazi wa taasisi mbili za nchi zenye nguvu, nazo ni Jeshi na Askari polisi.

Mwandishi akamtumia mhusika wa Koplo Marete katika Hadithi ya "Operesheni Kipindupindu", na kutoa maelezo ya kihistoria ya ufisadi wa mhusika huyu tangu kwanzoni mwa kazi yake Jeshini huku akisema: "Mwanzoni, alifanya kazi za kawaida za uanajeshi, baadaye akabahatika kuteuliwa kuwa mtunza ghala katika kambi yao, hapo ndipo alipojifunzia kongu zote za wizi na ulaji rushwa alizoea kutoa vitu ghalani na kwenda kuviuza kwa wenye maduka, askari walipopoteza au kuharibu vifaa vyao vya kikazi walimhonga na kupata vingine."⁽³⁰⁾

Na mwandishi ametoa maelezo haya kwa lengo la kubainisha historia yake akilitumikia Jeshi ambalo linatakiwa kuwa ndani yake na uwajibikaji na ufuataji wa sheria, kwa kuangalia hamu yake kubwa ya kutaka kujikusanyia fedha nyingi kwa njia mbali mbali zisizo za kisheria, alinuka ufisadi kwa kiwango ambacho ilikuwa ni vigumu kuinyamazia au kuikwepa, na kwa hiyo akafukuzwa kazini na kumuweka mbali na jeshi, baada ya kujichumia utajiri mkubwa tu wakati wa kazi yake jeshini. Na mwandishi akafasiri baada ya hayo,

namna ufisadi ulivyohama kutoka Jeshini kwenda katika katika sekta nyingine, akasema: "Alitumia kiasi kidogo cha pesa alizotoka nazo jesheni kununulia kazi katika manispaa ya Busola. Dira ya maisha yake ilikuwa ni ufisadi, aliamini kuwa pesa ziliweza kufungua milango iliyofungwa na kufuli elfu. Naam katika mazingira magumu ya ukosefu wa kazi, pesa zilimfungulia mlango wa manisapaa ya Busola, akapata kazi ya kusimamia kikosi cha askari wa manispaa hiyo." ⁽³¹⁾

Katika yaliyotangulia, inaonekana wazi namna gani Ufisadi ulivyotanda kutoka sekta kuelekea nyingine, na mwandishi hakujaribu kufupisha mazungumzo yake kuhusu ufisadi Jeshini, na ikawa athari yake ni finyu kwa watu katika maisha yao ya kila siku, lakini aliufanya kuwa unatanda na kuelekea katika eneo na kuathiri athari ya moja kwa moja katika maisha ya watu ya kila siku, na kubainisha athari ambazo huachwa na aina hii ya ufisadi dhidi ya idadi kubwa ya watu.

Na kutokana na sekta hizi ambazo zimeathirika kwa ufisadi wa mtu huyu, sekta ya mauzo ya chakula katika masoko ambayo yanauza vitafunio, viazi na vinginevyo na kwa bei ya chini mno kwa sehemu kubwa ya watu wa kipato cha chini na wafanyakazi ambao hali zao haziwaruhusu kujipatia chakula katika maeneo mengine ya bei ya juu, na katika hali za kuenea janga la kipindupindu, akina mama lishe walizuiliwa kufanya kazi zao za kuuza vyakula, na aliyekamatwa miongoni mwao hutiwa mbaroni, na haachiwi na kuondoka isipokuwa kwa kutoa rushwa kwa askari mhusika. Na mwandishi hakuishia hapo tu bali alibainisha kwa makusudi athari za askari huyu kwa akina mama lishe ambao walilazimika kuongeza bei za vyakula kwa ajili ya kulipia sehemu ya rishwa walioitoa kwa askari. Na mateso haya yalionekana wazi kwa wafanya kazi wa kipato cha chini ambao wanategemea kwa kiasi kikubwa chakula hichi cha bei ya chini, lakini hapakuwepo njia yoyote mbele yao isipokuwa kuufuata uhalisia na kukubali bei mpya za chakula. ⁽³²⁾

Na Ufisadi haukuishia katika kujikusanyia fedha tu kutoka kwa akina mama lishe wasiokuwa na uwezo, bali ilienea hadi kutwaa

chakula kinachobebwa na akina mama lishe hawa pale wanapokuwa hawana fedha zak utosha kutoa rushwa.⁽³³⁾

Mwandishi akaendelea kuuzungumzia ufisadi, sio tu katika sekta ya usalama bali akauzungumzia pia namna unavyosambaa hadi katika sekta zingine mbali mbali na kuathiri moja kwa moja maisha ya watu ya kila siku, na miongoni mwa sekta hizo ni ile ya usafi kwa mfano, hii ni sekta muhimu sana inayoyagusa maisha ya watu ya kila siku kwa njia ya moja kwa moja, na mwandishi akabainisha sura miongoni mwa sura za ufisadi wa sekta hii, huku akisema: "Usombaji wa takataka ulikuwa haufanyiki tena baada ya magari ya kufanyia shughuli hiyo kuporwa spea na wafanyi kazi wenye njaa." ⁽³⁴⁾

Ufisadi haujaishia katika sekta ya usafi tu bali ulienea katika sekta ya maji safi, nayo ni sekta ambayo watu hawawezi kuiepuka hata kwa dakika chache, na akatoa maelezo kwa yale mambo yanayojitokeza ndani ya sekta hii kwa kusema: "Wakazi wa mji sasa walikuwa wakinywa maji yasiyosafishwa kwa kuwa huduma ya usafishaji maji pia ilikuwa imekufa." ⁽³⁵⁾

Baada ya mwandishi kuzungumzia mrundikano wa takataka katika barabara mbali mbali na kuchafuka kwa maji ya kunywa, ilikuwa ni jambo la kawaida kwake kuhamia katika kuzungumzia athari zinazoachwa na hayo kwa watu wote, na kwa hivyo mwandishi akahamia katika kuzungumzia sekta ya afya na athari ya ufisadi katika sekta hii, na akatoa maelezo ya hayo akisema: "Hali ya hospitali kuu ya mji wa Bisula ni mbaya, na jokofu la chumba cha kuhifadhia wafu nalo liko katika hali mbaya mno, hakuna madawa hapo hospitalini, na pia hakuna vyakula. Vyumba vya wagonjwa vina msongamano kwa kuwa na idadi kubwa ya wagonjwa, kwa hivyo kila wagonjwa wawili wamelazwa katika kitanda kimoja na chumba cha kuhifadhia maiti kinatoa harufu inayozigonga pua kama mshale wa moto, na vifaa katika chumba cha kuhifadhia wafu vimekufa kama wafu wenyewe, na sehemu yote inanuka harufu mbaya mno"⁽³⁶⁾

Na hivi ndivyo mwandishi alivyoelezea hali ya mji mmoja kati ya miji ya nchi yake, na huwenda hii ikawa ni ishara kutoka kwa

mwandishi ya kuwa yanayotokea ndani ya mji huo yanazingatiwa kuwa ni mfano mdogo wa yanayotokea katika jamii nzima kwa ujumla. Kwa hivyo, huduma zinazotolewa kwa watu zimezorota kwa kiwango kinachoonekana, na huwenda sababu yake ishara ya mwandishi kwa watumishi mafisadi, hakuwataja majina yao au kazi zao mjini hapo, na kuwenda kwa ajili ya kujumuisha fikra yake kuhusu ufisadi unaokusanya sekta zote, na akasema kwa kuuelezea ufisadi huo kutoka kwa vigogo, ambao wamewafanya wale wadogo wawe wanafuata mwenendo wao, kwani mishahara yao kwa mfano haitolewi kwa nidhamu. Na sababu ni kama asemavyo mwandishi: "Hazina ya Manispaa ilikuwa imeporwa na genge la majambazi ambalo lilijiita maafisa wasimamizi wake pamoja na madiwani waliochaguliwa na wananchi." ⁽³⁷⁾

Na hivi ndivyo hali ilivyokuwa ndani ya mji huo, uliojaa wevi ambao wanabeba jukumu la yaliyotokea. Na huwenda kifo cha askari huyu Marete na cha Kiongozi wa mji huo baada yake katika ajali ya gari ni ishara ya kwamba huu ndio mwisho wa ufisadi. Na inaweza kuwa chaguo la kifo kama ni mwisho linaonesha hali ya kukata tama iliyompata mwandishi kutokana na marekebisho, na hivyo mauti yalikuwa ndio njia pekee inayoweza kuimaliza ufisadi.

Ubaguzi wa Rangi:

Waandishi wa nathari ya Kiswahili wamezoea kuashiria ubaguzi wa rangi na wamezungumzia mateso ya wananchi kutokana na uaguzi huu wa rangi. Isipokuwa mwandishi ameandika kuhusu jambo hili kupitia mwono wa mwingereza aliyeishi na kukulia nchini Kenya, na baada ya kuwasili kwa familia ya kiingereza kutoka Uingereza na kuja Nairobi, kwa lengo la kuanza maisha mapya katika nchi hii ambayo baashi yao walilizingatia kuwa ni nchi ya Wazungu (Kenya ni nchi ya Mtu Mweupe). Mtazamo huu wa kibaguzi ambao unawakilisha kizazi cha kale kilichoung'ang'ania. Na kuna kizazi kipya ambacho mwandishi amekieleza kuwa maisha yake yanatuama katika misingi mitatu mikuu: nayo ni kusadikika, Ukweli na Mantiki (Urazini), na mwandishi ameonesha katika Hadithi yake ya "Njozi ya Mtu Mweupe", yale mapambano kati ya kizazi kilichoona kuwa

mazuri ya Kusema kweli, Ukweli wenyewe, na mantiki ambayo inapaswa kuongoza, na kizazi kingeni kinaona kwamba: "Walikuwa na njozi, walitaka kuifanya Kenya nchi ya mtu mweupe na kwinginiko katika makoloni yake, ndoto hii ilikuwa na mashabiki wengi." ⁽³⁸⁾

Huu ni mtazamo wa baadhi ya waingereza kwa nchi nyingine yenye wananchi wenye kutarajia maisha bora zaidi, ingawa serikali ya Uingereza yenyewe iliamua kuangalia upya siasa zake kuelekea nchi ya Kenya, na kugeuza sera zake ambazo zilikuwa zikisema kwamba Kenya ni nchi ya Mtu mweupe, na hayo yalionekana wazi kwa kufanya marejeo ya Kiongozi mpya wa Kiingereza ambayo alizungumzia: "Alihubiri mahusiano mazuri miongoni mwa watu wa rangi tofauti tofauti, mwelekeo huu ulidhihirisha mabadiliko makubwa katika mawazo ya waingereza juu ya utawala wao katika koloni la Kenya." ⁽³⁹⁾

Ikiwa Serikali ya Uingereza ilianguka upya siasa zake za kikoloni nchini Kenya, kwa utashi wa kweli kwa ajili ya kuwapa wakenya haki ya kujiamulia wao wenyewe au kwa sababu nyingine mbali mbali, kwa hakika mwandishi ameelezea mwono huo ambao wakenya waliuona kwamba nchi yao ilikuwa ni ya Mtu Mweupe', akasema: "Sauti iliyonguruma mwanzoni mwa karne kuwa Kenya ni nchi ya mtu mweupe, sasa ilikuwa imedhoofishwa na mabadiliko makubwa ya kihistoria ambayo yalithibitisha kuwa sauti hiyo ilitoka kwenye kinywa cha kichaa aliyekuwa ndotoni." ⁽⁴⁰⁾

Mwandishi amesimulia mabadiliko ya fikra ya nchi kwanza, kisha akaweka wazi kwamba ingawa kuna mabadiliko haya aliyoyazungumzia, kuna wale wale ambao bado wanaendelea kuota ndoto hii ambayo imepitwa na wakati, na haiwezi tena kusimama kidete mbele ya uhalisia, nalo ni lile lililowakilishwa na Robert Stoneheart ambae alitoka London akiukimbia umasikini ambao haujamwezesha hata kujipatia elimu yake, na akaja nchini Kenya, akafanya biashara hadi akawa tajiri anaemiliki mashamba ya kahawa, na mwandishi ameelezea utajiri huu kupitia mwanae ambae alisema: "Maskani yetu mapya yalikuwa na nyumba kubwa iliyokuwa katika pembe ya shamba kubwa la mibuni la ekari thelathini, upande wa

kushoto kama mita mia mbili hivi kutoka nyumba yetu kulikuwa na vibanda kumi na vitano, humo ndimo walimoishi waafrika waliofanya kazi shambani." (41)

Hii ni ishara ya uhalisia mpya wa mhusika mwingereza aliyehamia Kenya kwa lengo la kutafuta maisha bora, na vile vile upeo wa kuboreka hali yake ya kiuchumi ukadhihirika. Na tofauti inayoonekana kati yake na kiwango cha maisha ya waafrika wenye ardhi, ingawa utajiri huu ulipatikana, mtazamo wa baadhi ya waingereza kwa waafrika haukubadilika, na mwandishi ameuzeza mtazamo huu kama ni ubaguzi kwa mujibu wa kauli yake: "Baada kulikuwa wazungu wahafidhina, kama Robert Stoneheart ambao walishikilia kwamba mzungu alikuwa binadamu bora kuliko binadamu wa rangi nyingenezo." (42)

Na hata kama kuna watu ambao bado wanauamini mtazamo huu wa kibaguzi kutoka Uingereza, wako miongoni mwao walioupinga mwelekeo huu, na wanajaribu kuivuka fikra hii iliyopitwa na wakati, kama vile mwelekeo huu wa daktari Welesh anaefanya kazi katika Hospitali ndogo iliyo karibu na shamba la Robert StoneHeart, akiwatibu watu wote; wa maumbile na rangi mbali mbali bila ubaguzi kwa sababu ya rangi au jinsia, na hili ni jambo lililomfanya Robert amwite daktari huyu "Daktari mjinga"! kwa nini anahimiza waingereza kuchanganyika na waafrika? Mimi kamwe siwezi kuwa na uhusiano na weusi kama nilivyokwambia mara nyingi... Weusi ni nyani ... epukana nao" (43)

Huu ndio mtazamo ambao baadhi ya watu wanaung'ang'ania na baadhi yaw engine kuukataa kabisa. Na bado kuna watu wanaendelea kushikilia mwono huu na hata wale ambao maisha yao yanamtegemea mtu mweusi kwa ajili ya kuongeza utajiri wake kama vile Robert stoneHeart aliyeelezewa kuwa ni: "Kadiri ilivyotajirika ndivyo chuki yake dhidi ya wanawake na watu weusi ilivyo zidi." (44)

Utajiri huu haujabadilisha mtazamo wa baadhi ya waingereza dhidi ya weusi, kama vile Robert StoneHeart, ambae aliendelea kumuusia mwanae kuufuata mtazamo huu anaounadi, na akakataa

mtoto wake kumfuata kwa ajili ya mageuzi ya kisiasa ambayo yanatoa nafasi kubwa ya wakenya kuiongoza nchi yao. Na uungaji mkono huu ukaelezewa kuwa ni aina yana baba akaendeleza msimamo wake hadi alipoiaga dunia. Na maneno yake ya mwisho kabisa yalikuwa: weusi ni nyani jiepuche nao! ⁽⁴⁵⁾.

Mwandishi ametaka kubainisha kuwa mwono huu wa kibaguzi bado upo, na una wanaouunga mkono lakini mtoto ambaye anawakilisha kizazi kipya ameukataa katakata mwono huu, na akaamini uhalisia na akili pamoja na ukweli ambao unakataa mwono huu, bali ukiongezea, kijana huyu alioa msichana wa kikenya, na ambae alimtoshelezea kila aina ya sababu za starehe na furaha. Na akajenga family yake kwa namna aliyoizingatia kuwa ni mwisho wa mafanikio ya mwono wake na fikra aliyokuwa akiinadi.

Mwisho:

Na anaazingatia kazi za uandishi wa Hadithi Fupiza Mbatiah anaweza kutoa idadi ya maangalizo na huwenda muhimu ya hayo ni:

-Familia na matatizo yake na mchango wake katika jamii, sura ya familia yenye migogoro, imekuwa ikijikariri mara kwa mara katika kazi za Hadithi fupi, na ikatumia nyakati za migogoro na kuangazia juu ya matatizo na masuala mbali mbali ya kijamii, yaliyo muhimu, na kuweka baadhi ya mitazamo kwa ajili ya kutafuta suluhisho la matatizo haya!

-Familia kwa Mbatiah, imekuwa na sifa ya kipekee, na kwa idadi ndogo inayowezezana, ya wanafamilia. Mara nyingi familia huundwa na Baba, Mama na mtoto mmoja, wawili kwa wingi. Na kuwepo kwa wavulana kumepindukia idadi kuliko wasichana. Ambapo pia uwepo wa mchango wa baba ulionekana wazi zaidi kuliko wa mama katik Hadithi hizi, na baadhi ya nyakati ikaonekana kutoweka kwa mchango wa mama, na huenda jambo hili linaashiria kuwa matatizo yaliyoibuliwa yanahitaji hekima na busara za baba pamoja na uwezo wake wa kurahisisha mambo.

-Sura ya watoto imekuwa ya aina mbali mbali katika familia; kwa hivyo akajitokeza mtoto mtiifu na mwenye nidhamu kwa kufuata maelekezo ya familia, napia mtoto mtukutu na mpinzani wa nidhamu ya familia, ingawa watoto wengi wa kiume ambao wanapendelea zaidi upande wa familia kama ngao yao inayowalinda kutokana na matatizo wanayokutana nayo. Na mwandishi hakuacha kubainisha mwisho wa Mtoto wa kiume mwenye nidhamu anaefuata maelekezo ya familia mara nyingi maisha yake huenda na kupita njia ya kawaida, na yule motto mtukutu ambaye mwisho wake unaweza kuwa janga na wakusikitisha, na katika jambo hili kuna wito wa kuzingatia hayo na kunufaika nayo na kumuhisisha msomaji faida za nidhamu na uwajibikaji wa maelekezo ya familia.

-Mwandishi ametumia mfano wa familia ya kiingereza na kuyaleta matukio ya Hadithi kamili kutokana na familia hiyo na hali zake nay ale yanayotokea ndani ya familia hiyo ikiwa Kenya, na akaweka wazi tofauti zilizopo kati ua muono na ufumbuzi wa matatizo kati ya familia mbili.

-Mwandishi ameitumia hali za afya za wanafamilia kama ni njia miongoni mwa njia za kuibualia hisia za wanafamilia wao kwa wao, na uwezo wa familia juu ya namna ya kushughulikia hali hizo.

-Elimu imechukua nafasi muhimu na kubwa nay a wazi katika Hadithi za Mbatiah, kwani yeye amefichua kwa uwazi mkubwa –na huenda kwa nguvu– msimamo wake kuhusu nchi kwa kuielekea sekta hii muhimu pamoja na wafanyakazi wake ambao amewaelezea kuwa ni mafukara, bali akafungamanisha kati ya anaefanya kazi katika sekta hii na umasikini kama vitu vinavyoambatana.

-Uzingatiaji mkubwa wa Hadithi za Mbatiah ulikwa katika elimu kwenye hatua zake za mwanzo, huenda ikawa, alihisi kuwa ngazi hizo ni za kipindi cha ukuzaji za utenenezaji na kinahitaji ari na malezi zaidi, japo kuwa haya hayamaanishi kuwa yeye hakuashiria masomo ya huo kikuu, bali aliyapa sehemu ya ari yake.

-Ari kubwa ya elimu kwa wavulana ilikuwa na umuhimu mkubwa katika kazi za uandishi wa Hadithi na hayakuonekana yanayohusu elimu ya wasichana isipokuwa katika kazi yake moja tu, na sababu yake inaweza kuwa ni kukosekana elimu kwa wavulana kuna kuwa na matokeo mabaya mno kuliko wasichana, nalo ni jambo aliloliandika katika Hadithi yake ya Sami.

-Mwandishi ameashiria ishara za mara kwa mara kushindwa kwa familia kushindwa kukamilisha elimu ya watoto wao wa kiume kwa sababu za kifedha zinazowakwaza wazazi wakashindwa kulipia masomo ya watoto wao. Na inaweza kuwa ishara iliyopo hapa inatoa wito wa kuangalia upya mfumo huu ambao baada ya kuutekeleza, umedhihirisha mabaya mengi yaliyoisumbua jamii yetu na bado yanaendelea kuisumbua.

-Ubaguzi wa Rangi nao umechukua nafasi yake katika Hadithi Fupiza Mbatiah, kwani ameutengea Hadithi kamili akizungumzia ndani yake maudhui hii kwa muono wake unaothibitisha kushindwa kwa fikra hii na kupingana kwake na akili pamoja na mantiki.

-Mwandishi amejaribu kuthibitisha kuwa ikiwa kuna anayeikanusha fikra hii, ngazi ya siasa na serikali, na kujaribu kuthibitisha kinyume chake na kwamba baadhi ya waingereza wanaendelea kuathiriwa na fundo hili la ubaguzi wa rangi.

-Mwandishi amegubua ugomvi ukinzani kati ya kizazi cha zamani ambacho baadhi yao wanaamini fikra ya ubaguzi wa rangi ambao unampa sifa mzungu na kumfanya bwana aliye juu ya wengine wote, na kizazi kipya – ndani ya nyumba moja – ambacho kinapinga na kukataa fikra hii, na kuongeza zaidi pale kizazi hichi kipya kinapozungumzia namna ya kuishi pamoja kati ya wazungu na waafrika bila ya kubaguana.

-Mbatiah alitenga pia sehemu ya kuonekana akizungumzia ufisadi na yanayotkana nao miongoni mwa athari zake mbaya zinazoigusa jamii katika sekta mbali mbali, na kwa hili, hatofautiani na waandishi wengine wengi wa nathari ya Kiswahili ambao wameuzungumzia ufisadi. Na akawaelezea wahusika mafisadi kwa pande mbili za jinsi walivyo na yaliyomo ndani yao, ispokuwa amekuwa peke yake kwa kutoa maelezo ya athari inayoachwa na ufisadi kwenye sekta mbali mbali na athari zinazofuatia kwa watu wote.

-Ni nadra kukuta kuwa kuna mwandishi anaeuashiria ufisadi katika taasisi ya Jeshi, miongoni mwa waandishi wa nathari ya Kiswahili. Kwa hivyo, aina mbali mbali za ufisadi daima hutuama kwa askari, vyama mbali mbali, na wafanyakazi wakubwa. Na inawezekana ikawa hii ni ishara ya kwamba sekta hii nayo pia haiku mbali sa ufisadi pamoja na ushujaa wa mwandishi.

-Mwandishi ametoa maelekezo kupitia mazungumzo yake, akiuzungumzia ufisadi ambao ameutengea Hadithi kamili kutokana na umuhimu wake – kutazamwa– kuwa watu wanatakiwa kuchungua undani wa kuwachagua wanaowawakilisha katika chaguzi mbali

mbali, kwani imeonekana kuwa wengi miongoni mwa hao wanashiriki kwa vitendo hasa katika ufisadi.

-Mbatiah ameelekeza uhakiki wake wa moja kwa moja na mkali kwa maafisa wanasisa na akawatuhumu kwa unafiki wao wa kisiasa, kwani wao huwaelekea watu kwa njia moja na kutendana nao kwa ufisadi na kwa njia inayothibitisha ushiriki wao wa wazi wazi.

الهوامش

1- Msokile, Mbunda (1991); Misingi ya hadithi fupi, Dar es Salaam University Press. Tanzania.

2- ----- (1993); Misingi ya Uhakiki Fasihi, East African Educational Publishers L.T.D. Nairobi.

-Mbatiah, Mwenda (2003);Mwongozo wa Wale Nisi, Longman Publishers, Nairobi.

-Njogo, Kimani (1997); Uhakiki wa Riwaya visiwani Zanzibar, Nairobi Unoversity Press, Kenya.

-Mohamed Said, Ahmed (1995); Kunga za Nathari ya Kiswahili; Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi, East African Educational publishers, Nairobi, Kenya. - Njogo, Kimani. Chimerah, Rocha (1999); Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Kenyea.

3- Mbatiah, Mwenda (2000); Kamusi ya Fasihi, Standard Text Books Graphics and Publishers, Nairobi Kenya.

-Wamitila, K. W. (2003); Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia, Focus Books, Nairobi, Kenyea.

- ----- (2003); Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi, Focus Books, Nairobi, Kenyea.

4- Mbatiah, Mwenda (2000); Arusi, Uk. 24

5- ----- " " Uk. 25

| | | | | |
|-----------|----------------------------|---------------------|---|---------|
| 6- ----- | " | " | " | Uk. 25 |
| 7- ----- | Kiumbe Hachukuliki | | | Uk. 80 |
| 8- ----- | " | " | | Uk. 79 |
| 9- ----- | (2007) Njozi ya Mtu Mweupe | | | Uk. 26 |
| 10- ----- | " | " | " | Uk. 32 |
| 11- ----- | " | " | " | Uk. 32 |
| 12- ----- | " | Kurudi Nyumbani | | Uk. 74 |
| 13- ----- | " | " | " | Uk. 74 |
| 14- ----- | " | " | " | Uk. 74 |
| 15- ----- | " | " | " | Uk. 78 |
| 16- ----- | " | " | " | Uk. 78 |
| 17- ----- | " | " | " | Uk. 22 |
| 18- ----- | " | " | " | Uk. 23 |
| 19- ----- | " | Sami | | Uk. 100 |
| 20- ----- | " | " | | Uk. 98 |
| 21- ----- | " | " | | Uk. 101 |
| 22- ----- | " | " | | Uk. 103 |
| 23- ----- | (2000); | Arusi, | | Uk. 12 |
| 24- ----- | (2000); | Kiumbe Hachukuliki, | | Uk. 74 |

| | | | | | |
|-----------|--------|--------------------------|---|---|-----------|
| 25- ----- | " | " | " | " | Uk. 83 |
| 26- ----- | (2007) | Kurudi Nyumbani, | | | Uk. 30 |
| 27- ----- | " | " | " | " | Uk. 90/91 |
| 28- ----- | " | Sami | | | Uk. 103 |
| 29- ----- | " | " | | | Uk. 103 |
| 30- ----- | (2000) | Operesheni Kipindupindu, | | | Uk.100 |
| 31- ----- | " | " | " | | Uk.100 |
| 32- ----- | " | " | " | | Uk.100 |
| 33- ----- | " | " | " | | Uk.105 |
| 34- ----- | " | " | " | | Uk.102 |
| 35- ----- | " | " | " | | Uk.102 |
| 36- ----- | " | " | " | | Uk.102 |
| 37- ----- | " | " | " | | Uk.101 |
| 38- ----- | " | Njozi ya Mtu Mweupe, | | | Uk.23 |
| 39- ----- | " | " | " | " | Uk.26 |
| 40- ----- | " | " | " | " | Uk.27 |
| 41- ----- | " | " | " | " | Uk.27 |
| 42- ----- | " | " | " | " | Uk.28 |
| 43- ----- | " | " | " | " | Uk.28 |
| 44- ----- | " | " | " | " | Uk.32 |

VITABU VYA MAREJEO:

1- Iribemwangi (2007); Alidhani Kapata, East African Educational Publishers L.T.D.

2- Mbatiah, Mwenda (2003); Mwongozo wa Wale Nisi, Longman Publishers, Nairobi.

3- ----- (2000) Mwendawazimu na Hadithi Nyingine, Jomo Kenyata Foundation.

4- ----- (2007) Kurudi Nyumbani na Hadithi Nyingine, Focus Publishers L.T.D.

5- Mohamed Said, Ahmed (1995); Kunga za Nathari ya Kiswahili; Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi, East African Educational publishers, Nairobi, Kenya.

6- Mbatiah, Mwenda (2000); Kamusi ya Fasihi, Standard Text Books, Graphics and Publishers, Nairobi Kenya.

7- MSokile, Mbunda (1991); Misingi ya hadithi fupi, Dar es Salaam University Press. Tanzania.

8- Madumulla, J.S (1995) Misingi ya hadithi fupi, kioo cha Lugha, na 1 Juzuu garida la kiswahilila isimu na fasihi, idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam

9- Mohochi (1998); Hadithi Fupi, utanzu uliopuuzwa, mulika, Na 24, Taasisiya uchunguzi wa Kiswahili, Dar-es-Salaam

10- Mohammed.S, A. (2005); Arusi ya Bulduze na Hadithi Nyingine, Longhorn Publishers LTD. Nairobi.

11- Njogo, Kimani (1997); Uhakiki wa Riwaya visiwani Zanzibar, Nairobi University Press, Kenya.

12- Njogo, Kimani. Chimerah, Rocha (1999); Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Kenya.

13- ----- (1993); Misingi ya Uhakiki Fasihi, East African Educational Publishers L.T.D. Nairobi.

14- Senkoro, F. E. M. K. (1998); Hadithi Fupiza Kiswahili, Lugha yetu, Toleo na 36, Baraza la Kiswahili la taifa, idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Dar -es- Salaam

15- Wamitila, K. W. (2003); Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia, Focus Books, Nairobi, Kenya.

16- ----- (2003); Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi, Focus Books, Nairobi, Kenya.